**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

Mobile: +255 -28-2810018
Fax: +255 - 28-2810701
E-mail: kasulutc@gmail.com
kasulutc@yahoo.co.uk

Chuo cha Ualimu Kasulu
S.L.P 3,
**KASULU.**

**Kumb: Na. KACCU/GFO/77/VII/....** 30, Juni 2025.



Ndg: ______________________________________

S.L.P. ________________________________

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU MWAKA 2025/2026**
***(Tafadhali soma maelekezo haya kwa makini kila kipengele)***

1. **UTANGULIZI**
Ninayo furaha kukuarifu kuwa, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekuchagua kujiunga na Mafunzo ya Ualimu kozi ya **Stashahada Maalum Elimu ya Msingi Sayansi, Hisabati na TEHAMA**. **Hongera sana**. Mafunzo haya ni ya miaka miwili (3). Aidha tunasisitiza kuwa uthamini uchaguzi huu uliopata kwa kuweka bidii katika masomo, kufuata taratibu na kanuni za chuo muda wote wa mafunzo.

2. **MAHALI CHUO KILIPO**
Chuo cha Ualimu **KASULU** kipo Mkoa wa **KIGOMA** Wilaya ya **KASULU.** Kipo kilometa 92 kutoka Kigoma Mjini na kilomita moja kutoka stendi kuu ya mabasi Kasulu, unaweza kufika kwa mguu au kwa kukodi bodaboda kwa gharama ya Tsh **1,000/=** tu.

3. **TAREHE YA KUANZA MAFUNZO**
Mafunzo kwa wanachuo wa mwaka wa kwanza yataanza **tarehe 18 Agosti, 2025.** Ripoti chuoni siku hiyo kwaajili ya usajili na kuanza rasmi mafunzo. Iwapo hutaripoti ndani ya wiki mbili kuanzia tarehe tajwa hapo juu hutapokelewa na utakuwa umepoteza nafasi hiyo. Mara baada ya kuwasili Chuoni fika ofisi ya **usajili** ukiwa na vitu vilivyoelekezwa, utapokelewa na kusajiliwa kwenye daftari la chuo.

4. **VYETI NA VIAMBATANISHO MUHIMU KWA USAJILI**:
   i). Fomu hii ya kujiunga na Chuo (Joining Instruction)
   ii). Cheti halisi (**original**) cha kidato cha nne. Result-Slip zitapokewa kwa wale tu waliomaliza mwaka 2025.
   iii). School Leaving Certificates za kidato cha nne, sita na ualimu.
   iv). Cheti cha kuzaliwa (**original**).
   v). Vivuli (Copy) za vyeti vyote vilivyotajwa hapo juu (ii-vi)
   vi). Faili 1 kwa usajili wako
   vii). Passport za watu wawili watakaoandikwa na kutambulika kama wazazi/walezi wako

viii). Medical Examination Form iliyojazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali (fomu imeambatanishwa mwishoni).

## 5. MALIPO YA MAFUNZO

### (a) ADA

Ada ya mafunzo ni **Tsh 450,000/=** kwa mwaka, Unatakiwa kulipa kiasi kisichopungua **Tsh 225,000/=** kwa kwa muhula ili upokelewe. Malipo ya Ada yafanywe kwa utaratibu wa CONTROL NUMBER. Kupata Control Number wasiliana na Mhasibu wa Chuo kwa Simu 0755410096 au 0694920594. **NB**: Risiti ya malipo (Bank Pay-in slip) utakabidhi ofisi ya usajili.

### (b) MICHANGO MBALIMBALI

| Na. | MCHANGO | KIASI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1. | Usajili na kitambulisho | 20,000/= | Kwa mwaka wa Kwanza tu |
| 2. | Kukodisha godoro | 10,000/= | Kwa mwaka |
| 3. | Usafi wa mazingira | 20,000/= | Kwa mwaka |
| 4. | Serikali ya wanachuo | 5,000/= | Kwa mwaka |
| 5. | Huduma ya kwanza | 10,000/= | Kwa mwaka |
| 6. | Michezo | 30,000/= | Kwa mwaka |
| 7. | Ulinzi | 30,000/= | Kwa mwaka |
| 8. | Ukarabati | 25,000/= | Kwa mwaka |
| | **JUMLA** | **150,000/=** | |

Michango yote ilipwe kupitia **Akaunti Namba 51403500048,** Jina la akaunti **KASULU T.C. PROJECT, Benki ya NMB.** Hati ya malipo ya Benki (Bank Pay-in slip) utakabidhi ofisi ya usajili.

## 6. SARE ZA CHUO

Sare rasmi kwa mwanachuo kwa muda wote wa masomo ni **Suti ya Dark Blue Kitambaa cha ESTIMU NAMBA 1**. Hakikisha sare inashonwa jinsi ilivyo elekezwa kuepuka kushona upya kama itakuwa tofauti. (Tazama picha za sare hapo chini kwa usaidizi).

| WANAWAKE | WANAUME |
|---|---|
| i). Sketi Dark blue mbili (2) zenye linda box mbele na urefu hadi karibu na viatu. | i). Suruali Dark blue mbili (2) zenye linda moja na turn-up chini. Upana wa chini usipungue **sm 16** |
| ii). Shati light blue mikono mirefu mbili (2) aina ya Kingsson au Kangaroo | ii). Shati light blue mikono mirefu mbili (2) aina ya Kingsson au Kangaroo |
| iii). Koti dark blue moja (1) lisilo na mpasuko. | iii). Koti dark blue moja (1) lenye vishikizo viwili na mipasuko miwili |
| iv). Tai dark blue ya kuishia kifuani baada ya kufungwa | iv). Tai dark blue ya kufika kiunoni baada ya kufungwa |
| v). Viatu vyeusi vya kufunika kisigino kifupi. | v). Viatu vyeusi vya kufunika kisigino kifupi. |
| vi). Soksi nyeupe | vi). Soksi nyeusi |
| | vii). Mkanda wa suruali mweusi wa ngozi. |

 

## 7. VIFAA MBALIMBALI

i). **Vifaa vya Taaluma**: Mihtasari ya masomo 2, Vitabu viwili (English Medium Class 4-6) vya masomo ya sayansi na hisabati, Kamusi ya Kiingereza, Daftari (Counter) zisizopungua 10, Kalamu za wino na penseli za kutosha, Mkebe wa Hisabati na Calculator.
ii). **Vifaa vya malazi**: Shuka mbili (Wanawake rangi ya pink & Wanaume rangi ya light blue), Mto na foronya mbili, Blanketi 1 na Chandarua.
iii). **Vifaa vya usafi**: Ndoo - 1 na Fagio la chelewa - 1.
iv). **Vyombo vya chakula**: Kontena 1 ya chakula yenye sehemu tatu, Kikombe 1, Kijiko 1, Galoni ya lita tano ya plastiki kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa.
v). **Vifaa vya michezo**: Tracksuit damu ya mzee yenye fito tatu, Jezzi damu ya mzee (T-shirtt na Bukta) Soksi pair 2 na Raba.
vi). **Vifaa vya Maabara**: Koti nyeupe kwa masomo ya Sayansi.
vii). Karatasi rimu 1 (photocopy A4) yenye karatasi 500. Aje nayo ofisini wakati wa kusajiliwa.
viii). **Nguo binafsi**: Nguo zingine zenye staha na zinazoendana na maadili ya kazi ya Ualimu unayoisomea, nguo za ndani za kutosha

***NB: Vifaa vyote hapo juu vitakaguliwa wakati wa kuripoti***.

## 8. MAHITAJI MENGINE MUHIMU YA MWANACHUO

i). Fedha tasilimu kwa ajili ya matumizi yake binafsi madogo madogo.
ii). Kadi ya Bima ya Afya ni LAZIMA kwa kila mwanachuo. Kama hana kadi atalipia Tsh **50,400/=** kwa ajili ya kukata Bima ya Afya ya mwanafunzi (NHIF).
iii). T- Shirt rangi ya right blue yenye nembo ya chuo (utaipata chuo baada ya kulipia Tsh. **15,000/=** kwenye akaunti ya michango iliyotajwa hapo juu.)
iv). Fedha ya mahafali Tsh. **10,000/=** aweke kwenye akaunti ya michango tajwa hapo juu
v). Fedha ya Joho Tsh. **20,000/=** aweke kwenye akaunti ya michango tajwa hapo juu
vi). Kufanya uchunguzi wa afya yake katika Hospitali za Serikali kwa kujaza medical examination form iliyoambatishwa mwishoni mwa maelekezo.

## 9. CHAKULA

Chuo hutoa chakula kwa wanachuo wote. Chuo hakina uwezo wa kutoa chakula maalumu (special diet) kwa wanachuo wagonjwa au mwanachuo mmoja mmoja.

## 10. SHERIA ZA CHUO NA KANUNI

Chuo cha Ualimu Kasulu kama ilivyo kwa vyuo vingine vya Ualimu, huendeshwa kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali za chuo na za nchi. Hivyo mwisho wa maelekezo

tumeambatanisha Sheria za chuo. Soma na kuzielewa kabla ya kuripoti chuoni. Pia utakapofika chuoni utapewa maelekezo ya ufafanuzi zaidi yatakayoamatana na ujazaji wa fomu ya kukubali kuzifuata kwa kipindi chote cha mafunzo haya.

**NB: Utapokelewa baada ya kukidhi maelekezo yote hapo juu.**

**MWISHO:** Jumuiya ya Chuo inakutakia maandalizi mema ya safari ya kuja chuoni.

KARIBU SANA CHUO CHA UALIMU KASULU

HELLEN M. CHEYO
MKUU WA CHUO

MKUU WA CHUO
CHUO CHA WALIMU KASULU
S.L.P 3
KASULU

NAKALA: Katibu Mkuu,
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S L P 10,
DODOMA.

Mkurugenzi Mafunzo ya Ualimu,
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S L P 10`
DODOMA.

Mthibiti Ubora Mkuu wa Shule (K)
Kanda ya Ziwa Magharibi
S.L.P 1185
KIGOMA

Afisa Elimu (M),
S.L. P 111
KIGOMA

Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Chuo,
S.L. P 3
KASULU

Kwa mawasiliano zaidi piga namba zifuatazo:-
0787322986 – Mkuu wa Chuo
0765124218 – Mwadili wa wanachuo
0754404423 au 0769 065874 au 0766310992 – Msajili wa wanachuo
0755352943 – Mratibu Taaluma wa Chuo

**GOVERNMENT OF TANZANIA**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**PART A:**

TO: The Medical Officer
……………………………………
……………………………………

From: Principal
Kasulu Teachers' College.

Please examine Mr/Mrs/Miss……………………………………………………………………………………..
To his/her physical and mental fitness for a full time teachers course.

A: 1. (a) Eye – sight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) Venereal Diseases
(e) Leprosy
(f) Limbs
(g) Epilepsy
2. Neuroses
3. Other serious diseases.

B: Blood Group

Date: …………………….. Signature………………………..

Official Stamp

---

**PART B:** **MEDICAL CERTIFICATE.**

(To be completed by Government Medical Officer)

I have examined the above named student that he/she is physically fit/unfit and mentally *fit/unfit for a full time teacher Education course.

I. (a) Eye – sight………………………………………………………
(b) Hearing…………………………………………………………...
(c ) Limbs…………………………………………………………
(d) Speech……………………………………………………………….
(e) Leprosy…………………………………………………………….

II. Neuroses…………………………………………………………………

III. Other serious diseases……………………………………………………………..

IV. Pregnancy……………………………………………………………….

**Date: ________________** **Signature __________________**
**Official Stamp**

## 11. AMBATANISHO LA NAKALA YA SHERIA NA KANUNI ZA CHUO, NA REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FORM

**SHERIA NA KANUNI ZA CHUO**:

Pamoja na maelekezo haya pokea sheria na kanuni za chuo ambazo utatakiwa kuzifuata wakati wote utakapokuwepo kwenye mafunzo, kama utaona ni ngumu kuzifuata Usije kwa sababu ndizo zinazolinda na kuhifadhi amani na utulivu kwa lengo la kuwezesha kila mwanachuo kufikia malengo yaliyokuleta hapa chuoni na taifa kwa ujumla.

**1.** i) Ruhusa kwa mwanachuo yeyote kwenda nje ya chuo muda wa masomo zitatolewa na mkufunzi wa zamu. Ruhusa za kulala nje ya chuo zitatolewa na Mkuu wa chuo kupitia ofisi ya Uadili.
ii) Ni kosa kwa mwanachuo kujiamulia kuondoka chuoni kwa muda mfupi au mrefu na kulala nje ya chuo pasipo ruhusa.

***(a) Mwanachuo atakayefanya kosa la kwenda nje ya chuo bila ruhusa kutoka ofisi husika au kuchelewa kurudi chuoni au kutoroka usiku, atapewa adhabu itakayopangwa pamoja na kuandikiwa barua ya onyo au kusimamishwa masomo kwa muda usiopungua siku kumi na nne (14).***
***(b) Aidha mwanachuo yoyote atakayeondoka chuoni kwa muda wa siku tisini (90) na kuendelea bila ruhusa ataachishwa chuo.***

**2.** i) Ni kosa kwa mwanachuo kutumia bangi, madawa ya kulevya, marijuana, mirungi na vitu vyote vinavyoendana na hivyo akiwa ndani na nje ya mazingira ya chuo. Aidha matumizi ya sigara hayaruhusiwi kwa mwanachuo.
ii) Pia ni kosa kwa mwanachuo kunywa pombe ya aina yoyote ile, mwanachuo atakaye kutwa na kosa hilo atafukuzwa chuo mara moja.
***Mwanachuo atakayekutwa na kosa la 2 (i) atafukuzwa chuo mara mojai. Aidha kwa mwanachuo atakayepatikana na kosa la 2 (ii) atapewa onyo kwa baruoa, adhabu yake atakayethibitika atafukuzwa chuo mara moja.***

**3.** Ni kosa kwa mwanachuo yeyote kumiliki au kushikilia silaha zinazoweza kuhatarisha usalama wa chuo na maisha ya wanajumuiya wa Chuo cha Ualimu Kasulu.
***Mwanachuo atakayekutwa na kosa hilo atapewa barua ya onyo, kupata adhabu itakayopangwa, kupelekwa polisi/kuachishwa chuo.***

**4.** i) Mavazi yanayotakiwa kuvaliwa na wanachuo wakati wote chuoni na nje ya chuo ni lazima yawe ya heshima, safi na yenye kulingana na mwongozo wa mavazi. Sare/Mavazi rasmi ya chuo itavaliwa wakati wote wa vipindi na mwanachuo anapotoka nje ya chuo.
ii) Kaptula, Nguo za mipasuo inayovuka magoti, Suruali za kubana, Suruali za jinsi, Sketi fupi, Kofia na malapa haviruhusiwi kuvaliwa na mwanachuo chuoni. Pia mwanachuo wa kike haruhusiwi kuvaa suruali akiwa chuoni isipokuwa sare ya michezo.
***Mwanachuo atakayebainika kuwa na makosa hayo atapewa onyo kali au adhabu au kusimamishwa masomo kwa muda usiopungua siku ishirini na moja (21).***

**5.** Ni kosa kuonesha unyanyasaji wa kijinsia au kimaumbile katika Chuo cha Ualimu Kasulu wa aina yoyote. Hii inajumuisha:
- i) Kumlazimisha mtu kwa kumtaka kimapenzi kwa kutumia maneno, ishara, picha au vitisho vyenye maudhui ya kimapenzi au kumsababishia mwanachuo kukosa amani ama kushindwa kuendelea na masomo yake.
- ii) Kutmia ishara za au kufanya mapenzi katika mazingira ya chuo.
- iii) Kumkashifu au kumnyanyapaa mtu yeyote kutokana na maumbile aliyonayo au ugonjwa alionao.

***Kwa mwanachuo atakayepatikana na kosa hilo atasimamishwa kuendelea na masomo kwa muda usiozidi siku ishirini na moja (21).***

**6.** Ni kosa kwa mwanachuo wa Chuo cha Ualimu Kasulu kujihusisha na ubakaji, ulawiti au usagaji.
***Mwanachuo yeyote atakayebainika kujihusisha na vitendo hivyo(a) atapelekwa kwenye vyombo vya sharia na akithibitika atafukuzwa chuo.***

**7.** Ni kosa kwa mwanachuo kujihusisha katika vitendo vya wizi chuoni na nje ya chuo, pia ni kosa kwa mwanachuo kujihusisha/kushiriki/kushawishi ugomvi nje au ndani ya mazingira ya chuo.
***Iwapo mwanachuo atapatikana na ikithibitika amevunja sheria hii ataachishwa masomo mara moja/atapelekwa polisi.***

**8.** Ni kosa kwa mwanachuo kupoteza au kuharibu kifaa au mali ya chuo kwa uzembe au kwa kukusudia ikiwa ni pamoja na kuandika au kuchora mahala pasipotakiwa kufanya hivyo au bila kibali cha kufanya hivyo kutoka katika uongozi wa chuo.
***Mwanachuo atakayetenda kosa hilo atalazimika kulipa fidia au kulipa kifaa husika.***

**9.** Ni kosa kushiriki kufanya vitendo vitakavyopelekea kumdhuru mtu au mali au mtu na mali yake katika mazingira ya chuo cha ualimu Kasulu.kosa hili ni kwa mwanachuo dhidi ya mwanachuo mwenzake, mfanyakazi na mwanajumuiya ya Chuo cha Ualimu Kasulu.
***Iwapo mwanachuo atatenda kosa hilo atatakiwa kulipa au kugharimia matengenezoya uhariibifu au madhala aliyosababisha au kusimamishwa masomo kwa muda usiozidi siku ishirini na moja (21).***

**10.** Ni kosa kwa mwanachuo kukataa kuhudhuria vikao/mikutano/mikusanyiko halali iliyoitishwa na uongozi wa chuo, kuitikia wito wa kuitwa na mfanyakazi halali wa Chuo cha Ualimu Kasulu, serikali ya wanachuo. Aidha ni kosa kutoshiriki katika kazi zilizopangwa na uongozi wa chuo, serikali ya wanachuo au wakufunzi wa Chuo cha Ualimu.

MKUU WA CHUO
CHUO CHA WALIMU KASULU
S.L.P 3
KASULU